



TANGAZO LA MAENEO YA KUPANGISHA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na.	ENEO	KAMPASI/MAHALI	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Kampasi ya Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano	Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano	Mgahawa mdogo wa chakula (Idadi ya wateja kwa siku ni 50 - 70)
2.	Hosteli za Ubungo	Chumba kilichopo ndani ya Kantini	Steshenari

Kwa tangazo hili, UDSM kinawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma hizo. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 228 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi Elfu Kumi Tu (**TZS 10,000/=**) kupitia 'Namba ya Kumbukumbu' ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe **23 Februari 2023** itakuwa ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi waombaji wote wanatakiwa kuwepo katika Hosteli za Ubungo na saa 6:00 mchana wanatakiwa kuwepo katika Kampasi ya Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika, waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo ya maombi yao kwa njia ya barua.

IMETOLEWA NA
NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA
15.02.2023